Yesu amedhihirisha ya kwamba Mungu sio hakimu aliyekasirishwa nasi na anayetafuta nafasi ya kutuhukumu. Bali Mungu kwa hiari yake na kutokana na upendo wake kwetu alimtoa mwanae aje awe mwokozi mtawala wetu (Yohana 3:16-17). Baada ya kazi ya Yesu duniani kuisha, yeye na Mungu baba walimtuma Roho Mtakatifu kusimika upendo wa Mungu ndani ya mioyo yetu, ili kutubadili na kutuongoza kuingia maisha ya ukamilifu.

***Tumaini hilo haliwezi kutuhadaa, maana Mungu amekwisha miminia mioyoni mwetu upendo wake kwa njia ya Roho Mtakatifu aliyetujalia.***
*(Warumi 5:5,)*

## *Je, tunapaswa kufanya nini?*

Hatupaswi kufanya lolote kupokea neema ya Mungu tusiostahili (Waefeso 2:8-9), bali kama zawadi yoyote tunayopewa inastahili kupokelewa kwa shukrani. Je, tunapaswa kupokea hii zawadi vipi? Angalia jibu la Yesu kuhusu hilo:

***"Wakati umetimia, na Ufalme wa Mungu umekaribia. Tubuni na kuiamini Habari Njema!"***
*(Mariko 1:15)*

Maana ya kutubu ni kubadili mawazo, kuacha kutegemea tumaina lisilo la kweli, usalama na utabulisho usio wa kweli, na kuanza kumtegemea Mungu, kuweka tumaini letu kati Kristo na ufalme wake wa amani, raha na utengamano. Maana ya kutubu kuacha kuishi katika giza la dhambi na kuanza kuishi katika mwanga wa upendo na msamaha wa Mungu.
Kuamini ni ni kuweka tumaini letu lote na tunavyomiliki kwa Kristo, kufuata njia zake za upendo, na kuendelea kukuza uhusiano kati yetu na yeye.

*27Akajibu akasema, Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote, na kwa akili zako zote; na jirani yako kama nafsi yako.*

*(Luka 10:27)*

Unaweza kuanza kumfuata Kristo na njia yake ya upendo kwa kuanza na ombi kama ifuatavyo:

*Ahsante Baba wa Binguni kwa kuonyesha pendo lako kwangu, ahsante kwa kunifanya mwanao, ahsante kwa kumtuma mwanao Yesu Kristo awe mwokozi wangu kwa kuziondoa dhambi, dhiki na aibu yangu. Ahsante kwa upendo na msamaha uliounyesha kwangu katika Kristo.*

*Ahsante Mungu wa rehema kwa kumtuma Roho Mtakatifu aishi moyoni mwangu, shuka Roho wa Mungu – Niongoze katika ukweli wa Mungu.*

*Nifunze kumpenda Mungu na watu wengine,*
*Nipe msukumo na nguvu ya kufuata njia ya Kristo.*

*Katika jina la Yesu nimeomba, AMEN.*

Katika kuhusiana kwa njia hii na Mungu kwa maombi, umeingia katika maisha ya uhusiano wa kudumu na Baba, Mwana na Roho Mtakatifu – safari ambayo itabadili maisha yako hatua baada ya nyingine. Kupitia kwa Roho Mtakatifu, Yesu atatuoongoza pamoja na wengine kumfuata na kumwabudu Mungu kulingana na mapenzi yake kama yalivyoandikwa kwenye Biblia. Hauko peke yako.

***Hii ndio habari njema – kwako wewe na ulimwengu wote!!!***

Hii kabrasha imetolewa na Grace Communion International. Kushiriki katika moja ya kanisa zetu katika eneo lako tembelea tofutti:
www.gci.org.au/home/connections/congregations.aspx
Or Namba ya simu: 07 5553 6000

Kujifunza zaidi kuhusu habari njema kwako wewe na ulimwengu wote tembelea tofuti:
http://www.gci.org/gospel/everyone.

All scriptures, unless noted otherwise, are quoted from the Holy Bible, New International Version®. NIV®. Copyright ©1973. 1978. 1984.

# *Hii ni habari njema kwa kila mwanadamu*

**Grace Communion International**

*Living and sharing the gospel*

## *Hii ni habari njema kwa kila mwanadamu!*

*"Roho wa Bwana yu juu yangu. Amenichagua kuwahubiria maskini Habari Njema. Amenituma kuwatan gazia wafungwa kuwa wako huru, kuwaambia vipofu kuwa wanaweza kuona tena; na kuwaweka huru wanaoonewa, na nitangaze mwaka ambao Bwana atawabariki watu wake."*
*(Luke 4:18-19, The Message)*

Mungu Baba alimtuma mwanae wa pekee Yesu Kristo ili kudhihirisha upendo wake kwetu. Yesu hakutuletea habari njema tu ya ufalme wa Binguni bali yeye ndiye habari njema kwa wanadamu wote na wewe pia umeshirikishwa!!

***Maana Mungu aliupenda ulimwengu hivi hata akamtoa Mwana wake wa pekee, ili kila amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.***
*(Yohana 3:16)*

Ni Yesu pekee anaweza kutufundisha upendo wa Mungu kwa kuwa yeye kama mwana wa pekee, ni yeye pekee anayemfamu Mungu binafsi tangu mwanzo (Mathayo 11:27). Kupitia neno lake kama lilivyoandikwa kwenye Biblia, Yesu ametufunza kuwa Mungu ni Baba anayetupenda na sisi ni wanae anaowapenda.

*Tazameni jinsi Baba alivyotupenda mno, hata tukaitwa watoto wa Mungu! Na hivyo ndivyo tulivyo. Watu wa ulimwengu hawatutambui kwa sababu hawakumjua Mungu. (1 Yohana 3:1)*

Kabla ya kuumba ulimwengu, Baba yetu wa binguni aliamua kutuumba kama wanae wapendwe – "Aturithi" ili tuwe sehemu ya familia yake, akiwa na nia ya kutushirikisha kwenye uhusiano uliokamili kati ya Mungu na sisi na wanadamu wengine.

*3 Asifiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo ambaye ametu bariki sisi kwa kila baraka za kiroho zitokazo mbinguni tukiwa ndani ya Kristo. 4 Mungu alituchagua sisi tuwe ndani ya Kristo hata kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu, watu wasio na lawama mbele zake. 5 Kwa upendo wake, alipanga kabla ya mambo yote, kutufanya sisi kuwa watoto wake kwa njia ya Yesu Kristo kwa mapenzi yake mwenyewe; 6 na hivyo apewe sifa kwa ajili ya neema yake tukufu ambayo tumepewa bure katika Mpendwa wake.*

*(Waefeso 1:3-6)*

Pamoja na kwamba tangu mwanzo ulikuwa mpango wa Mungu kutushirikisha na kuturithi, sisi wanadamu (Kwa kuanzia wanadamu wa kwanza kuumbwa) tumeasi huo mpango, na viumbe vyote vime adhiriwa na dhambi hiyo kwa miaka yote.

Kwa kuzingatia hiyo nia ya kuturithi tuwe wanae, Mungu Baba kwa neema alimtuma mwanae aje aishi miongoni mwetu kama mmoja wetu. Akiwa pamoja na Baba yake katika nia, Yesu alishuka na akaje ali awe sehemu yetu milele.

*Neno akawa mwanadamu akaishi kati yetu akiwa amejaa utu kufu na kweli. Tuliona utukufu wake, utukufu wa Mwana pekee wa Baba.*

*(Yohana 1:14)*

*Alipochukua umbo la mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii mpaka kufa, tena kifo cha msalaba. (Wafilipi 2:8)*

Kama mwakilishi wetu, kwa hisani yetu, Yesu aliishi maisha ya upendo uliokamilika, imani na utii ili wanadamu wote wapate urejesho kwa Mungu na waokolewa kutoka kwenye minyororo ya dhambi, kifo na nguvu za ouvu. Yesu alikuja kufuta madhara ya dhambi, ili kurekebisha na kuweka kila kitu sawa.

Pamoja na kwamba tuliumbwa ili tuwe na uhusiano wa kina na Mungu, hakuna hata mmoja anayemwamini Mungu na upendo wake kikamilifu. Wote tumechagua kutoheshimu Mungu na mpango wake kwa maisha yetu.

*kwa maana wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu; (Warumi 3:23)*

Badala ya kumwamini Mungu na kupokea upendo wake wa pekee, tumetafuta maisha, upendo, maana na hifadhi katika maisha kwa njia zetu. Matokeo yake ni ulimwengu wa majuto. Pamoja na kwamba bado upendo wa Mungu unadhihirika, lakini mara nyingi maisha yanaonekana yasiyo na maana, kama tumepotea na yasiyoweza kurekebishika.

Lakini Mungu hakupoteza nia yake ya kwanza kwa viumbe vyake. Aliamua kuingilia kati ili kuviokoa – kwa gharama yake mwenyewe na bila hata kuzingatia upinzani kutoka kwa wanaookolewa. Mungu aliamua kuchukua mzigo wetu wa dhambi tulizotenda, na zilizotendwa dhidi yetu, akafanya lolote linalowezekana kutufanya viumbe wapya.

Pamoja na kuwa wote tumeanguka, na kutenda dhambi, Mungu alidhihirisha upendo wake mkuu kwetu kwa kumtuma mwanae Yesu Kristo aje, afe msalabani katika mikono ya waovu. Yesu kwa kupenda kwake na bila chuki aliyatoa maisha yake kugharimia maisha yetu ya dhambi.

*Lakini Mungu anaudhihirisha upendo wake kwetu kwamba: tulipokuwa tungali wenye dhambi, Kristo ali kufa kwa ajili yetu.*
*(Warumi 5:8)*

Ni maisha ya Yesu pekee ambayo yangeweza kuangamiaza kifo ambazo kilikuwa kinatukabili. Ni Yesu pekee, mwana na Mungu milele, ambaye anaweza kurejesha uhusiano ulikuwa umevunjika kati ya Mungu na wanadamu. Gharama walioingia Mungu Baba, Mwana na Roho Mtakatifu kwa ukombozi wetu kutoka kwenye minyororo ya dhambi zetu, na kutoka kwenye kifo, inastahili.

Kwa niaba yetu, Yesu alikandamiza kifo, uovu na akafufuka na hatakufa tena. Ndani yake tumepata urejesho katika uhusiano kamili na Mungu. Ndani yake tunaishi milele.

Baada ya ufufuko wake wa pekee, Yesu alirejea kwa Baba yake, akaahidi kuwa atarudi duniani siku moja, aje aufanye bingu na dunia ambapo wote tutakuwa sawa na Mungu. Lakini kwa sasa anafanya maandalizi kwa niamba yetu, aturejeshe kwa Mungu, ili tuweze kupata urejesho wa milele katika upendo wa neema na upendo wa Mungu Baba.

*Katika nyumba ya baba yangu mna nafasi nyingi. Kama sivyo, nisingeliwaambia kwamba nakwenda kuwaandalia makao. 3 Na nikishawaandalia, nitarudi kuwachukua mkae pamoja nami; ili mahali nilipo, nanyi mpate kuwepo.*
*(Yohana 14:2-3, SNT)*